*SWAHILI FORUM 12 (2005): 121-132*

# VITENDAWILI VYA KISWAHILI: USAMBAMBA WAKE NA DHIMA YAKE KATIKA JAMII[1]

DEO NGONYANI

## 1. Utangulizi

Vitendawili vya Kiswahili, kama vitendawili katika lugha nyingine za Kibantu, na kwa hakika katika lugha nyingine za Kiafrika, ni mafumbo ambayo hutolewa kama kauli au swali linalotaka jibu (Gowlett 1979; Harries 1971, 1976; Okpewho 1992). Tutaiita kauli ya swali kisabiki[2], na kauli ya kufumbua tutaiita jawabu. Kitendawili kifuatacho ni mfano mzuri.

(1) Kisabiki: Nyumba yangu haina mlango. (Farsi #6)[3]
Jawabu: Yai!

Katika mfano huu, fumbo lililo katika kisabiki lazungumzia nyumba. Lakini nyumba hiyo si kama nyumba tunazozifahamu kwa sababu haina mlango. Ili kutegua kitendawili hiki, anayejaribu kutegua lazima atambue kwamba maelezo ya nyumba yana kitu kisicho cha kawaida kwa nyumba. Jambo hili ndilo dokezo la jawabu. Majawabu ya vitendawili vingi hukubalika hasa kimapokeo tu, na siyo hasa kutokana na mantiki. Kwa sababu hiyo mtu hujifunza kitendawili kama kitu kimoja (Blacking 1961: 5).

Kama ilivyo katika lugha nyingine za Kiafrika, vitendawili katika Kiswahili ni sehemu muhimu sana ya michezo ya watoto. Katika jamii ambazo bado zinaishi maisha ya jadi, watoto hukaa pamoja jioni pengine wakiwa na dada zao, kaka zao, na binamu zao wakasimuliana hadithi na kutegeana vitendawili. Aghalabu kunakuwa na zawadi za kubuni kama vile miji kwa mtoaji kitendawili ambacho wasikilizaji wameshindwa kutegua. Hata hivi leo huko Afrika ya Mashariki unaweza kusikia vitendawili vikitegwa katika programu za watoto katika redio, na mashuleni.

Wachunguzi wengi wa tanzu hii ya fasihi simulizi wameviangalia zaidi vitendawili kama mchezo tu wa watoto. Hii imepelekea wengi wao kuhitimisha kwamba umuhimu wa vitendawili ni mchezo hasa na havistahili kupata muda mwingi sana wa kuvichunguza (Finnegan 1977; Okpewho 1992; Blacking 1961). Okpewho (1992), kwa mfano, anasema:

---

[1] Makala haya yalitolewa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Masomo ya Kiafrika (African Studies Association), New Orleans, 13 Novemba, 2004. Nawashukuru sana wote waliohudhuria katika jopo letu na kwa mchango wa mawazo. Shukurani zaidi kwa Bwana Patrick Malloy kwa mchango wa pekee. Shukurani pia zimwendee aliyepitia makala hii kwa niaba ya wahariri na kunishauri juu ya mambo mbalimbali.

[2] Neno *kisabiki* linatokana na kitenzi *kusabiki* kinachomaanisha kutangulia. Uchambuzi mwingi wa vitendawili umeiita kauli ya kwanza ‘precedent.’ Katika makala hii tunatumia *kisabiki* kama tafsiri ya neno hili la Kiingereza na siyo swali kwa sababu si kila kauli ya mwanzo yenye muundo wa swali.

[3] Tutatumia vitendawili kama vilivyoandikwa katika kijitabu cha Farsi (1958) na kamusi ya Ndalu na Ikambili (1991).

> *Although they have attained some status of excellence through long use and bear the same mark of sensitive observation of life and nature as the proverb, they are used primarily for entertainment, or play. We shall, therefore, spend less time on them than we have done on proverbs.* (Okpewho 1992: 239).
>
> Ijapokuwa vitendawili vimepata umaarufu kutokana na matumizi ya muda mrefu na vinaonesha kuwa vinatokana na uchunguzi wa maisha na asili kama zilivyo methali, vinatumika hasa kwa madhumuni ya burudani, au mchezo. Kwa hivyo, tutatumia muda mchache zaidi kuliko tulivyofanya na methali.

Hapana shaka kwamba msisitizo wa upande wa mchezo na burudani katika vitendawili ndiyo uliopelekea vitendawili kutochunguzwa zaidi ukilinganisha na tanzu nyingine za fasihi simulizi. Tunadiriki kusema kwamba vitendawili havijaeleweka vema, na umuhimu wake haujatambuliwa ipasavyo.

Makala hii inachunguza muundo wa visabiki vya vitendawili vya Kiswahili na kutokana na mchangamano wa muundo tunapendekeza kwamba vitendawili ni njia kuu ya kufundishia watoto ufasaha wa lugha. Muundo wa vitendawili umejengwa juu ya usambamba (*parallelism*) katika ngazi mbalimbali za muundo wa lugha. Usambamba ni kanuni kuu ya tanzu mbalimbali za fasihi (Jakobson 1987b). Ukichunguza usambamba katika vitendawili utaona changamoto kubwa hutolewa kwa mtegaji na wasikilizaji wake kutokana na usambamba ulioko katika sintaksia, fonolojia, kadhalika sitiari. Kwa kuwa michezo ni njia bora sana ya kufundishia watoto, vitendawili vimetokea kuwa changamano na vyenye umuhimu mkubwa. Kama Scheub (2002: 124) asemavyo: "Vitendawili ni modeli kwa ajili sanaa za lugha."

Hoja hii juu ya umuhimu wa usambamba inatolewa katika sehemu tano zifuatazo. Katika sehemu ya pili ya makala hii, maelezo na ufafanuzi juu ya dhana ya usambamba yanatolewa. Sehemu ya tatu inafafanua usambamba wa kisintaksia na kifonolojia katika vitendawili vya Kiswahili. Mifano ya usambamba uliopo katika sitiari, yaani usambamba wa kisemantiki, inajadiliwa katika sehemu ya nne. Katika sehemu ya tano, mjadala unajaribu kuunganisha dhana ya usambamba hasa wa kisemantiki na umuhimu wa sitiari katika kukuza ufasaha wa lugha. Tutajaribu kutetea hoja kwamba dhima kuu ya vitendawili hasa ni kuwatayarisha watoto katika stadi za lugha fasaha, kujenga uzoefu wa matumizi ya tamathali za usemi katika lugha ya kawaida, na kuwaandaa katika kutumia mantiki na analojia. Sehemu ya sita inatoa muhutasari na inahitimisha mjadala na maoni yaliyopo katika makala hii.

## 2. Usambamba

Kwa miaka mingi, usambamba umetambuliwa kuwa ni kanuni kuu ya mitindo na miundo katika mawanda na tanzu mbalimbali ya fasihi. Usambamba unafasiliwa kwa kifupi kuwa ni mlandano wa muundo. Muundo huo unaweza kuwa wa kisintaksia, mofolojia, au fonolojia (Fabb 1997: 137). Inaaminika kwamba neno hili lilianza kutumiwa kama istilahi ya fasihi na Bwana Robert Lowth ambaye aliandika:

> *The correspondence of one Verse, with another, I call Parallelism. When a proposition is delivered, and a second is subjoined to it, or drawn under it, equivalent, or contrasted with it, in Sense; or familiar to it in the form of Grammatical Con-*

> *struction; these I call Parallel Lines; and the words or phrases answering one to another in the Corresponding Lines, Parallel Terms.* (Robert Lowth kama alivyonukuliwa na Jakobson 1987a: 146)
>
> Mshabaha wa aya moja na nyingine, ninauita usambamba. Kauli moja inapotolewa, na ya pili ikaunganishwa, au ikawekwa chini yake, ikalingana, au ikatofautishwa nayo katika maana; au ikafanana nayo katika muundo; ninaiita misitari hiyo misitari sambamba; na maneno au virai vinavyojibizana katika misitari inayoshabahiana, virai sambamba

Lowth aliandika maneno haya baada ya kuzichunguza aya za Biblia na kugundua jinsi ambavyo zilirudiarudia miundo fulani. Katika miaka ya karibuni, wanazuoni wengine wameanza kuuangalia upya usambamba, na kugundua kwamba usambamba ni msingi wa miundo na mitindo ya tanzu mbalimbali za fasihi (Jakobson 1983, 1987a, 1987b). Jakobson aliandika:

> *There is a system of steady correspondences in composition and order of elements on many different levels: syntactic constructions, grammatical functions and grammatical categories, lexical synonyms and total lexical identities, and finally combinations of sounds and prosodic schemes. This system confers upon the lines connected through parallelism both clear uniformity and great diversity.* (Jakobson 1983: 102-103).
>
> Kuna mfumo wa mshabaha katika tungo na katika mfuatano wa elementi katika viwango mbalimbali: viambajengo vya kisinktasia, uamilifu wa kisarufi na kategoria za kisarufi, usawe wa kileksia na maana za jumla, na mwisho mchangamano wa sauti na mipango ya arudhi. Mfumo huu unaipa misitari iliyounganishwa kwa usambamba ulinganifu na anuai.'

Kwa mujibu wa Lowth, kuna aina tatu za usambamba: (a) mfanano wa kauli ambapo kile kisemwacho hurudiwa kwa kutumia maneno yanayofanana; (b) usambamba unaotokana na tabaini (antithetical) ambapo misitari inayoshabahiana inaeleza mkinzano (opposition); na (c) usambamba katika muundo. Usambamba katika muundo unaelezwa hivi:

> *Structural parallelism holds between two sections of text when they are the same at some level of structure (for example, when they have the same phrase structure).* (Fabb 1997: 137)
>
> Usambamba wa muundo hutokea baina ya sehemu mbili za matini (text) zinapokuwa sawa katika kiwango fulani cha muundo (kwa mfano, kunapokuwa na muundo sawa wa virai)

Kufanana huko kunaweza kuwa katika sintaksia, mofolojia, au fonolojia. Mfanano wa kisemantiki huonekana vizuri sana katika sitiari kwa sababu kwa asili sitiari zinafananisha vitu vinavyoshabahiana.

Fabb (1997) anaelezea kwamba usambamba una kazi kuu tatu. Kwanza, usambamba ni kanuni ambayo hufanya matini kuwa na muundo. Kwa mfano vina na mizani katika ushairi ni namna mojawapo ya usambamba. Katika mashairi ya Kiswahili, vina na mizani ndiyo hupambanua mashairi hayo siyo tu kutoka nathari, bali pia aina mbalimbali za mashairi. Kazi nyingine ya usambamba ni kile Jakobson alichokitaja kuwa ni kuvuta uzingativu kwenye matini "Poetics deals primarily with the question 'what makes a verbal message a work of art?'" Jakobson (1987b: 63). "Tanzu za fasihi hujihusisha hasa na swali 'ni kitu gani kinachofanya

ujumbe wa lugha kuwa sanaa?'" Usambamba hufanywa na marudio ambayo hufanya ruwaza ivutiayo. Kazi ya tatu ya usambamba ni kuelezea mtazamo wa kiutamaduni juu ya uwili katika dunia. Kama tutakavyoona, vitendawili kwa asili yake na kwa jina lenyewe huundwa kwa uwili. Uwili huo hutokana na tamathali za usemi, sitiari na mfanano wa maumbile ya vitu mbalimbali katika dunia.

Matumizi ya usambamba wa sitiari yanaweza kueleweka vizuri zaidi kama tutatumia mtazamo wa kiisimu. Mtazamo mpya wa kiisimu umeonesha kwamba sitiari ni muhimu katika lugha ya kila siku (Lakoff na Johnson 1980; Lakoff 1990; Turner 1990). Kwa mujibu wa mtazamo wao, sitiari huundwa kwa mawanda mawili: (a) mawanda ya tajriba yanayozungumziwa, na (b) mawanda ambayo maneno yake hutumika kuelezea mambo yanayozungumziwa (Lakoff na Johnson 1980: 5). Mawanda ya kwanza mara nyingi huwa ni dhahania and mchangamano na huitwa mawanda yalengwayo. Mawanda ya pili kwa kawaida ni ya mambo thabiti na yaliyozoeleka zaidi, nayo huitwa mawanda chanzo. Kwa hakika sitiari hazihusu jozi moja tu ya maneno. Dhana nyingi na maneno yanayohusiana katika mawanda ya kileksia hufanya mshabahiano wa mawanda ya sitiari. Ili kuelewa sitiari ipasavyo yampasa mtumiaji wa lugha kulinganisha maneno katika mawanda yote mawili[4].

Hebu tuangalie mfano mmoja kutoka lugha ya kila siku. Mara kwa mara tunasikia maneno kama:

*Tumetoka mbali, ameaga dunia, mgeni amewasili, vuka vikwazo, kupiga hatua*

Misemo yote hiyo inaelezea kusafiri au kutembea katika maana yake ya msingi. Lakini misemo hiyo hutumika kuzungumzia maisha. Kwa hivyo mawanda chanzo kwa maneno hayo ni *safari*, na mawanda yalengwayo ni *maisha*. Mara nyingi sana tunazungumzia maisha kuwa ni safari, na watu ni wasafiri. Uhusiano wa maneno haya mawili hauishii katika jozi hii tu bali katika jozi nyingi. Mshabaha wa sitiari za Maisha ni Safari unaonekana hivi.

| **Chanzo** | **Lengo** |
|---|---|
| safari | →maisha |
| aga dunia | →kufa |
| mgeni | →mtoto mchanga |
| kuwasili | →kuzaliwa |

Kuelewa sitiari na kutumia sitiari ni kuunda mshabaha wa maneno ya mawanda hayo mawili.

Kutokana na mifano hii twaweza kuona kwamba ufahamu wa sitiari unatokana na uhusiano fahiwa. Kwa mujibu wa uhusiano fahiwa tunatambua kuwa kila neno linahusiana na maneno mengine mengi katika mawanda. Kwa mfano, *aga, wasili, vuka,* na *mgeni* ni maneno

[4] Mtazamo wenye mawanda mawili tu siyo mtazamo pekee katika isimu ya lugha au katika mtazamo wa kiutambuzi. Wanazuoni wengine wamependekeza kwamba kuna mawanda mengi. Turner na Fauconnier (1995), kwa mfano, wanapendekeza mawanda mengi na wanashauri kwamba mawanda mawili ya Lakoff na Johnson yaangaliwe kama sehemu ya mawanda mengi. Katika makala hii tunatumia mawanda mawili kwa sababu ni msingi bora wa kuelewa usambamba.

yanayopatikana katika mawanda ya safari. Maneno haya yanapotumika kuelezea *maisha*, yanafahamika kirahisi kwa sababu uhusiano fahiwa katika mawanda ya safari huhamishiwa katika mawanda ya maisha. Kwa sababu hiyo basi, maneno katika mawanda haya mawili huonyesha usambamba. Vitendawili, kwa asili yake, huweka sambamba maneno ya mawanda mawili katika kuunda mafumbo.

## 3. Usambamba wa Miundo ya Vitendawili.

Sehemu hii inachambua mfanano wa muundo wa sentensi na usambamba wa kifonolojia katika kisabiki. Uchambuzi huu utadhihirisha kwamba kuna aina nyingi za usambamba wa kisintaksia na kifonolojia. Tutaona namna chache tu katika makala hii.

### 3.1 Usambamba wa Kisintaksia

Kabla ya kuangalia mifano ya usambamba wa kisintaksia katika vitendawili, hebu tuuone muundo wa sentensi za Kiswahili. Kiswahili ni lugha ambayo ina muundo wa Kiima-Kitenzi-Yambwa (SVO). Sifa mojawapo muhimu ya Kiswahili, kama lugha nyingine za Kibantu, na upatanisho wa kisarufi ambao huhusisha viambajengo vingi vyenye nomino.

Kuna vitendawili vinavyoundwa na kishazi kimoja (yaani sentensi sahili), na kuna vitendawili vinavyoundwa na zaidi ya kishazi kimoja (yaani sentensi changamani). Pia kuna vitendawili vinavyoundwa na sentensi ambatani. Mifano ifuatayo inaonyesha vitendawili vya sentensi sahili.

(2) Kuku wangu katagia mayai mibani. (Farsi #11) →nanasi

(3) Ubwabwa wa mwana mtamu. (Farsi #8) →usingizi

Mfano wa kwanza ni wa sentensi sahili ambayo ina kiima (kuku wangu), kitenzi (katagia) na yambwa yake ya asili (mayai) na mahali (mibani). Sentensi ya pili ni mfano wa kishazi kisicho na kitenzi. Ina kiima (ubwabwa wa mwana) na kiarifu (mtamu).

Vitendawili vingi sana vinaundwa na sentensi ambatani. Sentensi hizo zinaweza kuwa na kiunganishi kama *na, lakini*, au *bali*, na pengine huunganishwa na mkato tu. Kitendawili kifuatacho ni cha sentensi ambatani.

(4) Nyumba yangu kubwa bali ina nguzo moja tu. (Farsi #28) →uyoga

Vishazi viwili vilivyounganika ni *nyumba yangu kubwa* (kishazi kisicho na kitenzi), na *ina nguzo moja* (kishazi chenye kitenzi). Vishazi hivi vinaunganishwa na *bali*. Sentensi zinazounda vitendawili vya namna hii huwa na muundo unaofanana.

Vitendawili vya sentensi changamani huundwa na kishazi kikuu chenye kishazi bebwa. Kwa mfano:

(5) Ninapompiga mwanangu watu hucheza. (Farsi #13) →ngoma

(6) Anataga huku akitambaa. (Farsi #31) →mboga

Katika (5), kishazi kikuu ni *watu hucheza*. Kishazi bebwa ni kishazi elezi *ninapompiga mwanangu*. Kishazi bebwa hiki huelezea wakati. Muundo wa (6) unaonesha kwamba kishazi kikuu kinaundwa na kitenzi *anataga*, nacho kinafuatiwa na kishazi elezi *huku akitambaa*.

Usambamba wa kisintaksia huonekana kirahisi sana katika vitendawili ambayo huundwa na sentensi ambatani. Vishazi vinavyounda sentensi ambatani hii hufanana katika muundo wake. Mifano ifuatayo unatupa picha ya usambamba huo.

(7) Maiti wanasema bali waliochukua wamenyamaa kimya.
(Ndalu na Ikambili #434) →chungu na mafiga

(8) Nikija kwenye ndege wanifukuza na nikienda kwenye wanyama hawanitaki.
(Ndalu na Ikambili #622) →popo

Katika mfano (7), kishazi cha kwanza kina Kiima-Kitenzi, hali kadhalika kishazi cha pili kina Kiima-Kitenzi. *Kimya* ni kielezi katika kishazi hicho. Licha ya usambamba huu wa muundo, kitendawili hiki kina kinguanishi *bali*, ambacho kinaashiria kwamba kauli zinazounganishwa zina mkinzano. Hii ni aina mojawapo ya usambamba kama ilivyoainishwa na Lowth kuwa ni usambamba wa tabaini. Aina hii ya usambamba huonekana mara kwa mara kwa sababu kila kisabiki kinatoa kauli ambayo inaashiria kwamba kinachosemwa siyo kinachomaanishwa. Mfano (8), unaonyesha pia sentensi changamani mbili zinazounganishwa na kunganishi *na*. Sentensi zote mbili zina vishazi bebwa ambavyo ni vishazi sharti. Sentensi hizo ni *Nikija kwenye ndege* na *nikienda kwenye wanyama*. Baada ya vishazi hivyo kuna vishazi vikuu *wanifukuza* na *hawanitaki*. Hii ni mifano ya mfanano wa miundo.

### 3.2 Usambamba wa Kifonolojia

Usambamba wa kifonolojia hujidhihirisha katika ruwaza zinazohusu sauti, kiimbo, toni, kiinitoni, mkazo, na mpangilio wa silabi. Mfanano wa kifonolojia huimarisha usambamba unaoonekana katika mawanda mengine ya lugha. Mfano mzuri wa usambamba wa kifonolojia ni vina katika mashairi na katika nyimbo. Marudio ya sauti au silabi fulani hupambanua aina za mashairi[5].

Katika vitendawili vya Kiswahili, kuna vingi ambavyo vinatumia usambamba wa kifonolojia. Matumizi ya vina au marudio ya silabi fulani ni aina moja ya mfanano unaozungumziwa. Mifano mitatu ifuatayo ina usambamba unaotokana na kurudia silabi.

(9) Haukamat<u>iki</u> wala haushik<u>iki</u>. (Farsi #58) →moshi

(10) Kitendawili changu cha aj<u>abu</u> kina matone ya dhah<u>abu</u>. (Farsi #7)
→qurani takatifu

(11) Kisimani kwa Bi-Mp<u>aji</u>, kuna jini mnywa m<u>aji.</u> (Farsi #54) →taa ya mafuta

[5] Mokitimi (1996) anaandika kwa kirefu juu ya usambamba wa kisintaksia na kifonolojia na anatoa mifano mizuri katika vitendawili vya Kisotho.

Katika mfano (9), sauti *–iki* zinatumika kumalizia vishazi viwili vinavyounda kitendawili hicho. Katika (10), *-abu* inaonekana mwishoni mwa kiima na yambwa. Kadhalika, katika (11), kielezi kinaishia na *–aji*, na mwisho wa sentensi kuna *–aji* tena.

Vitendawili tulivyoviangalia vinaonesha marudio ya sauti fulani ambazo ziko katika maneno yanayofahamika vizuri tu. Vitendawili vingine vingi vina marudio ya sauti ambazo si sehemu ya maneno ya kawaida, bali idiofoni au onomatopia.

(12) Ukiona 'Njigi' utadhani 'Njege'; na unapoona 'Njege' utafikiri 'Njigi'. (Farsi #22) →maziwa na tui la nazi

(13) Huku 'Ngo' na kule 'Ngo'. (Farsi #43) →giza

(14) Nikiita 'baba' huitika 'baba'. (Ndalu na Ikambili #621) →mwangi

Vitendawili hivi vitatu vinatumia marudio ya sauti kama idiofoni. Kila idiofoni ikiangaliwa peke yake, haileti fumbo lolote wala ujumi wala uvutivu wowote. Ikirudiwa katika muundo ulio sambamba kuna ujumi unaoongezeka. Kwa sababu hiyo marudio na ruwaza ni muhimu sana (Mokitimi 1996).

## 4. Sitiari katika Vitendawili

Katika sehemu ya pili ya makala hii, usambamba ambao ndiyo asili ya sitiari ulijadiliwa. Katika sehemu hii tunaangalia jinsi sitiari zilivyo muhimu katika kuunda mafumbo ya vitendawili. Tutaona kwamba kisabiki kinatoa maneno yahusuyo mawanda chanzo, na pia maneno yanayoonekana katika mawanda yalengwayo. Nyongeza ndogo hufanywa ili kuonesha kwamba ingawa kuna usambamba wa maneno katika mawanda mawili, kuna sifa au maneno ambayo si sahihi kwa mawanda yalengwayo.

Hebu tuangalie muundo wa sitiari katika kitendawili: *Maiti wanasema bali waliochukua wamenyamaa kimya*. Mawanda haya mawili yanaweza kuonyeshwa hivi.

| **Kisabiki** | **Jawabu** |
|---|---|
| mazishi | →jiko |
| wachukuzi | →mafiga |
| maiti | →sufuria, chungu |
| kusema | →kufanya kelele, sauti |

Tumeona kwamba kuna vitendawili vingi ambavyo mkinzano huashiriwa na maneno kama *lakini, bali*, na kadhalika. Katika kitendawili hiki mkinzano huo unaonekana katika kioja kilichopo ndani yake. Hatutegemei maiti kusema. Lakini katika kitendawili hiki, si tu kwamba maiti anasema, bali pia waliombeba wako kimya. Maneno katika mawanda haya mawili yanadhihirisha ulinganifu fulani ambao ndiyo usambamba tuuzungumziao. Usambamba huu umejipanga barabara.

Vitendawili vingi vina usambamba usio kamili. Yaani, baadhi ya maneno hayana ulinganifu. Aghalabu, kiunganishi kinachoashiria kutokamilika kwa ulinganifu hutumika. Lakini mara

nyingi hakihitajiki. Kitendawili tulichokiona awali, *nyumba yangu haina mlango*, ni mfano mzuri.

| **Kisabiki** | **Jawabu** |
|---|---|
| nyumba | →yai |
| nafasi ya kuishi | →nafasi ya kuishi |
| kuta | →ganda |
| mlango | →ø |

Katika mfano huu, mfanano wa *nyumba* na *yai* unaonekana kana kwamba mtu anasema kwamba yai ni kama nyumba isiyo na mlango. Kama ilivyo katika nyumba, kuna nafsi inayoishi katika ganda la yai. Walakini, kama huyo anaeyeishi katika nyumba hiyo isiyo na mlango akitaka kutoka nje je? Basi lazima ataivunja nyumba ili atoke. Wazo hili linaweza kumpelekea mtu kutegua kitendawili hicho.

Kwa hivyo, sitiari ni muhimu sana katika kufumba au kutega vitendawili. Mshabaha wa maneno katika mawanda ya sitiari ni muhimu sana kwa kuunda usambamba. Sitiari pia ni sababu kubwa ya kuwepo vitendawili kwani ni njia muhimu ya kuwafunza watoto tamathali za semi kama tutakavyoona katika sehemu ifuatayo.

## 5. Dhima ya Vitendawili Katika Jamii

Wataalamu wengi waliochunguza vitendawili vya Kiafrika wamedai kwamba madhumuni makuu ya vitendawili ni mchezo wa kujiburudisha watoto (kwa mfano, Blacking 1961, Finnegan 1977). Katika sehemu hii tutazijadili hoja zilizotolewa kuthibitisha madai haya, na halafu tutajaribu kuzingatia mchango wa methali katika makuzi ya watoto.

Hoja kuu ni kwamba vitendawili hufanywa wakati wa michezo. Wataalamu hao hutoa kama ushahidi ukweli kwamba katika jamii nyingi watoto huamriwa kutotegeana vitendawili wakati wa mchana au wakati wa kazi (Blacking 1961). Amri hii imefasiriwa vibaya. Kuzuia watoto kutofanya mchezo wa vitendawili mchana kuna sababu kubwa mbili za msingi. Sababu ya kwanza ni kuwafunza watoto kufanya vitu kwa wakati wake. Kuna wakati wa kazi na wakati wa kucheza; kuna wakati wa sherehe na wakati wa kusikitika. Vitendawili vina wakati wake. Sababu ya pili ni kuzuia watoto wasisahau shughuli nyingine muhimu za siku ili kutegeana vitendawili. Ikumbukwe kwamba katika makabila mengi, amri ya kufanya vitu kwa wakati wake haihusu vitendawili tu. Masimulizi ya hadithi pia hukatazwa saa zisizo zake.

Miongoni mwa Wandendeule wa kusini Tanzania, mwandishi wa makala hii aliishi chini ya amri kama hizo. Watoto waliamriwa kutosimuliana hadithi wala kutegeana vitendawili saa za mchana. Na kama kawaida ya mafunzo ya wakati huo, tuliambiwa kwamba tabia ya kufanya hadithi na vitendawili wakati wa mchana inaweza kupelekea mtoto kuota mkia. Licha ya kwamba mkia ni kitu kisicho cha kawaida na kioja kwa mwanadamu, lakini pia mkia ni kitu kinachouma sana kama tunavyoweza kuona katika sugu ya nyuma ya nyani. Baada ya kupata umri kidogo, kaka zetu na dada zetu walitueleza kwamba hivyo vilikuwa vitisho ili tusiharibu

kazi kwa sababu ya hadithi. Hebu fikiri, kwa mfano, vijana wachungapo mbuzi, kwa mfano. Iwapo watakaa na kusimuliana hadithi, wataacha mbuzi wazagae na kula mahindi katika mashamba ya watu. Hii ndiyo sababu hasa ya kuzuia watoto wasifanye hadithi na vitendawili wakati wa mchana. Kwa sababu kuna vitu vingine vya kufanya na kila kitu lazima kifanyike kwa wakati wake.

Hoja ya pili dhidi ya madai kwamba vitendawili hufundisha watoto mantiki na analojia, ni kwamba hakuna ushahidi kwamba watu hujifunza mantiki katika vitendawili, kama Cole-Beuchat (1957) anavyodai. Blacking (1961) alifanya utafiti kujaribu kuthibitisha kama ni kweli kwamba ujuzi wa vitendawili unaakisi ufahamu wa mantiki, analojia, na kadhalika. Kwa mujibu wa utafiti wake, hakuna ushahidi wowote kwamba watu wenye ujuzi mkubwa wa vitendawili walikuwa weledi pia katika stadi nyingine za kiutambuzi. Lakini uchunguzi huo haukuzingatia mchango wa vitendawili katika kutambua tamathali za semi, methali au sitiari ambazo watoto walijifunza kutokana na vitendawili.

Hoja ya tatu ni kwamba analojia na mantiki ya kila kitendawili ni kitu kinachokubalika katika jamii, na si lazima kitambulike hivyo katika jamii zote na lugha zote (Harries 1971; Blacking 1961). Jibu la vitendawili hujulikana kama kitu kimoja (Blacking 1961). Ufumbuzi wa kitendawili kwa kiasi kikubwa hautegemei uwezo wa mtu kutambua au kukumbuka maana ya kila taswira na tafsiri yake. Ufumbuzi wa kitendawili unatokana na kujua mtego na jibu lake. Maana nyingine zinawezekana kimantiki. Kuna vitendawili vyenye maana zinazoelezeka vizuri, na kuna zile ambazo maana zake hazitokani na analojia nzuri sana. Vitendawili vyenye anaolojia nzuri zaidi hudumu kwa muda mrefu zaidi (Harries 1971: 386). Lakini kutaraji kwamba watoto wadogo wanoacheza na vitendawili wataweza kufahamu analojia na kutumia analojia vizuri kama vile wenye uzoefu mkubwa wa kutumia analojia si matarajio sahihi. Badala yake, kuna vitendawili ambavyo baada ya matumizi ya muda mrefu, watoto huanza kuona na kutambua tamathali za usemi, sitiari na anolojia zilizofichika.

Matumizi ya vitendawili muda mrefu hupelekea kutambua mambo kadha katika matumizi ya lugha yakiwemo tamathali za usemi, sitiari, utata, na busara za wahenga katika misemo. Matumizi ya vitendawili huwatayarisha watoto kuanza kuzoea sitiari. Sitiari hazifundishwi kwa kuoneshwa bayana kwa watoto kwamba hii ni sitiari na maana yake ni hii. Lakini baada ya kucheza vitendawili kwa muda mrefu watoto wanaweza kutambua kwamba katika matumizi ya lugha, wakati mwingine maneno na misemo itumikayo huweza kumaanisha kitu kingine katika mawanda tofauti kabisa. Katika jamii nyingi methali ni kitu muhimu sana katika ufasaha wa lugha. Tunaweza kukumbuka alivyoandika Achebe kwamba methali ni kama mawese ambayo huungiwa katika maneno yasemwayo (Achebe1959: 7). Vitendawili huwatayarisha watoto kutumia maneno kwa uangalifu na busara.

Methali, kama vitendawili, huficha busara za wahenga. Kile kilichosemwa na Blacking (1961) kuwa ni upungufu katika vitendawili kwa hakika ndiyo nguzo ya vitendawili. Kama tulivyosema awali, fumbuzi wa kitendawili hutegemea kukijua na kukikumbuka kitendawili chenyewe na jibu lake na siyo kutatua au kukokotoa mantiki yake. Kitendawili hudumu kwa

sababu ya mantiki na analojia yake. Ubora wake unatokana na busara ya waliotunga. Kadhalika, methali ni misemo ya kimapokeo. Methali na vitendawili vinafanana sana kutokana na umuhimu wa usambamba na sitiari. Methali ni majumui yanaofunza, yanayoonya, na yanayotahadharisha (Shapin 2001). Vitendawili havina dhima hizo. Lakini vitendawili na methali vina asili moja ya utata. Ukikichukua kitendawili chochote na kukichanganua kwa mujibu wa mantiki na analojia yake, bila shaka utaona kwamba mantiki yake haina mshikamano na wala si sahihi sana. Jambo hili hudhihirika katika methali pia. Kama Shapin anavyoonya, ingawa methali zinakusudia kutoa mawazo ya majumui juu ya jambo fulani, katika lugha zote methali zina mkinzano na kasoro katika mantiki yake (Shapin 2001: 751). Kwa hivyo si busara kuichambua methali nje ya muktadha wa matumizi halisi. Kwa mfano:

(15) Haraka haraka haina baraka.

(16) Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako.

Methali mbili hizi zinaonekana kupingana. Lakini watumizi wazuri wa methali wanajua wakati gani wa kutumia methali ya kwanza na wakati gani kutumia methali ya pili. Jambo hili ni muhimu kwa watoto kujifunza pia. Katika vitendawili, watoto hufunzwa kuzoea utata na mantiki isiyo kamili. Lakini hujifunza pia juu ya busara za kimapokeo.

Kudumu kwa methali kunatokana na kuwa na sitiari ambazo zinaonesha usambamba mzuri. Kwa mfano:

(17) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

(18) Hapana masika yasiyo na mbu.

Twaona katika methali ya kwanza marudio ya silabi. Jambo lililo muhimu ni kwamba jambo lisemwalo si hasa kuvunjika mguu, bali jambo baya litamtokea mtu asiyesikia la mkuu. Kadhalika methali ya pili haizungumzii masika na mbu kwa hakika, bali kila neema huja na dhiki zake kama vile mvua na mbu. Mvua ni neema kwa sababu hukuza mimea na chakula. Mvua pia husababisha madimbwi ambamo mbu hutaga na kuzaliana. Mbu ni chanzo kikubwa cha dhiki kwani siyo tu kwamba ni wadudu wanaokera sana wanapowauma binadamu, bali pia wanaeneza magonjwa mabaya sana. Methali hii inatoa muhutasari wa habari nyingi kwa kutumia tamathali za usemi. Ili kuelewa tamathali hizi za usemi, mtu anahitaji kuzoea matumizi mbalimbali ya lugha. Aristotle alitahadharisha kwamba misemo ya kimapokeo huwafaa wazee kwa sababu wana tajriba pana na kwamba haifai kwa watoto kutumia hiyo (Aristotle 1982: 9). Kwa hivyo basi, matumizi ya vitendawili huwatayarisha watoto kutumia lugha kwa ufasaha zaidi, ufasaha ambao huonekana vizuri sana katika matumizi ya methali na nahau.

Dhima nyingine kubwa ya vitendawili ni kuwahimiza watoto kuyachunguza mazingira na kuuona usambamba katika maumbile ya asili. Kwa mfano: *Nikija kwenye ndege wanifukuza na nikienda kwenye wanyama hawanitaki* (NI #622). Jawabu lake, kama tulivyoona, ni *popo*. Kiumbe hiki kinaweza kufikiriwa kuwa ni ndege au ni mnyama. Popo ana mabawa na anaruka kama warukavyo ndege. Lakini pia anaonekana ana umbile kama la panya mnyama. Kitendawili hiki hakitoi ufumbuzi wa kama popo ni ndege au mnyama. Lakini hapana shaka

yoyote watoto wataanza kufikiri, je, ni ndege au mnyama? Methali hii ina lengo la kuchochea udadisi na si kumstarehesha tu mtoto.

Kwa hivyo basi, dhima kuu ya vitendawili katika jamii ni kuwafunza watoto staid za lugha kwa kutumia mchezo.

## 6. Hitimisho

Makala hii imezungumzia usambamba katika vitendawili. Kwa kutumia mifano ya usambamba wa kisintaksia, kifonolojia, na sitiari, tumejaribu kutoa hoja mbili muhimu. Hoja ya kwanza in kwamba usambamba ni muhimu sana katika kutega vitendawili na kuwa ni msingi wa ruwaza. Hoja ya pili ni kwamba vitendawili ni njia muhimu sana ya elimu ya jadi kwa sababu vitendawili vinawatayarisha watoto katika matumizi ya lugha fasaha na methali mbalimbali. Ni muhimu kusisitiza matumizi ya vitendawili tena katika elimu ya watoto kama njia mojawapo ya kudumisha busara za wahenga.

## Marejeo


Achebe, Chinua 1959. *Things Fall Apart*. New York: Anchor Books Doubleday.

Aristotle 1982. *Rhetorics XXII*. Tafsiri ya John Henry Freese. Cambridge, Mass.: Harvard University Press

Blacking, John 1961. The Social Value of Venda Riddles. *African Studies* 20,1: 1-32.

Cole-Beuchat, P-D: 1957. Riddles in Bantu. *African Studies* 16,3: 133-149.

Fabb, Nigel 1997. *Linguistics and Literature*. Oxford: Blackwell Publishers.

Finnegan, Ruth 1977. *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Georges, Robert A. & Alan Dundes 1963. Toward a Structural Definition of the Riddle. *Journal of American Folklore* 76: 111-118.

Gowlett, D. F. 1979. A Structural Typology for Bantu Riddles. *African Studies* 38,1: 47-65.

Farsi, S. S. 1993. *Swahili Sayings 2: Riddles and Superstitions*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Harries, Lyndon 1971. The Riddle in Africa. *Journal of American Forlklore* 84: 377-393.

Harries, Lyndon 1976. On the deep structure of riddles. *African Studies* 35,1: 39-43.

Jakobson, Roman 1983. *Dialogues*. Tafsiri ya Kiingereza na Krystyna Pomorska. Cambridge, Mass.: Massachusetts Institute of Technology.

Jakobson, Roman 1987a. Grammatical parallelism and its Russian facet. *Language and Literature*, imehaririwa na Krystyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge, Mass.: Belknap Press of Harvard University Press. Uk. 145-179.

Jakobson, Roman 1987b. Linguistics and poetics, *Language and Literature*, imehaririwa na Krystyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge, Mass.: Belknap Press of Harvard University Press. Uk. 62-94.

Lakoff, George & Mark Johnson 1980. *Metaphors We Live By*. Chicago: Chicago University Press.

Mokitimi, Makali I. 1996. The Sesotho Riddle as a Poetic Text. *South African Journal of African Languages* 16,3: 96-100.

Ndalu, Ahmed E. & Hanrietta M. Ikambili 1991. *Kamusi ya Vitendawili na Mafumbo.* Nairobi: Heinemann Kenya.

Okpewho, Isidore 1992. *African Oral Literature*. Bloomington: Indiana University Press.

Scheub, Harold 2002. *The Poem in the Story: Music, Poetry, and Narrative*. Madison: The University of Wisconsin Press.

Shapin, Steven 2001. Proverbial Economies: How an Understanding of Some Linguistic and Social Features of Common Sense Can Throw Light on More Prestigious Bodies of Knowledge, Science for Example. *Social Studies of Science* 31,5: 731-769.

Turner, Mark & Gilles Fauconnier 1995. Conceptual Integration and Formal Expression. *Metaphor and Symbolic Activity* 10,3: 183-204.